

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

Simu. Na.: +255(026)-2963114/115
Barua Pepe: ps@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz
(Barua zote ziandikwe Kwa Katibu Mkuu)



Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
S. L. P 2996,
40478 DODOMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na: CGA.68/157/01

11 Oktoba, 2022

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

Yah: **MALALAMIKO YA MWEKEZAJI KAMPUNI YA AL HUSHOOM
INVESTMENT (T) Ltd**

Tafadhali rejea somo lilitajwa hapo juu

2. Wizara imepokea barua ya tarehe **07 Oktoba, 2022** kutoka kwa mwekezaji Kampuni ya Al Hushoom Investment (T) Ltd kuhusu kuchelewa kupatiwa cheti cha Uwekezaji. Katika barua hiyo, mwekezaji ameeleza kutoridhishwa na huduma inayotolewa na ofisi yako katika kushughulikia suala lake la kupewa cheti cha TIC kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa usafirishaji wa mizigo (Delays for the issuance of TIC certificate of extension for the execution of the cargo transportation project). Aidha, mwekezaji huyo ameeleza kufuatilia mara kwa mara upatikanaji wa cheti hicho bila mafanikio.

2. Utakumbuka katika kikao cha 34 cha Kamati ya NISC Mhe. Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa alielekeza kutowakwamisha wawekezaji katika kutekeleza miradi yao. Aidha, alisisitiza Serikali kutokuwa sababu ya wawekezaji kushindwa kutekeleza miradi yao.

3. Kwa barua hii unaelekezwa kuhuisha cheti hicho na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji Wizarani ifikapo tarehe **14 Oktoba, 2022**. Pamoja na barua hii, nimeambatisha nakala ya barua kutoka kwa mwekezaji huyo kwa urahisi wa rejea.

3. Tunashukuru kwa ushirikiano wako.


N. G. Maregeli
Kny: KATIBU MKUU